# TARGETER KCPE JARIBIO LA PILI STAHIKI
## DARASA LA NANE - 2021

**STAHIKI 002**

# KISWAHILI:
# SEHEMU YA KWANZA:
# LUGHA

**Muda: Saa 1 Dakika 40.**

### MAAGIZO KWA WATAHINIWA
### SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1-50, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali: Fuata maagizo kujaza swali hili.**

**18.** Kisawe cha hulka ni ____________

A. ubaya.
B. mawazo.
C. tabia.
D. upungufu.

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

| 16. | [A] [B] [C] [D] | 17. | [A] [B] [C] [D] | 18. | [A] [B] [-C-] [D] | 19. | [A] [B] [C] [D] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|

**18,** kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja** tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

*Huchapishwa na kuratibiwa na taasisi ya uchapishaji ya Targeter Educational Publishers Ltd.*
*Email: info@targeterpublishers.co.ke*

**GEUZA UKURASA**

***<u>Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.</u>***

__1__. Hii ni methali inayopigiwa mfano mtu aliyepewa madaraka__2__hayawezi kwa kuwa hana __3__zinazohitajika. Pendo,__4__kuwa kisomo chake__5__kidigi, alijipata__6__hadi kuwa mhasibu mkuu.__7__uongozi wake, wale waliohudumu chini yake waliweza__8__za shirika husika bila kujali. Uchunguzi ulipofanywa, lawama__9__zilimwangukia yeye kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake ilivyopaswa. Kumbe alipata cheo hicho kwa__10__.

**1.** **A.** Ndugu ni kufaana si kufanana **B.** Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki
**C.** Kichwa cha kuku hakistahili kilemba **D.** Mwana wa ndugu kirugu mjukuu mtu wa mbali

**2.** **A.** ambazo **B.** ambayo **C.** ambalo **D.** ambavyo

**3.** **A.** hekima **B.** mikakati **C.** ilhamu **D.** stadi

**4.** **A.** licha ya **B.** kwa kuwa **C.** kwa vile **D.** kwa sababu

**5.** **A.** ilikuwa **B.** kilikuwa **C.** zilikuwa **D.** vilikuwa

**6.** **A.** akishushwa cheo **B.** akipigwa msasa **C.** akikwezwa cheo **D.** akipigwa mafamba

**7.** **A.** Nje ya **B.** Karibu na **C.** Juu ya **D.** Chini ya

**8.** **A.** kuvunja pesa **B.** kufuja pesa **C.** kuvuja pesa **D.** kuwekeza pesa

**9.** **A.** zote **B.** yote **C.** lote **D.** vyote

**10.** **A.** kula vya mwiku **B.** kupigwa kumbo **C.** kuzunguka mbuyu **D.** kula jasho lake

Lugha ya Kiswahili ina sauti__11__. Baadhi ya sauti hizi huwa sauti sighuna mathalani__12__. Lugha hii pia ina tamathali kadhaa kama vile istiari. Mfano wa istiari ni__13__. Ni jambo la kuonea__14__kuona kuwa thumni saba yaani__15__ya wanafunzi wanamudu lugha ya Kiswahili.

**11.** **A.** thelathini **B.** thelathini na moja **C.** tano **D.** ishirini na tao

**12.** **A.** ch, f, s, th **B.** gh, j, m, t **C.** p, ny, n, d **D.** dh,k,ng,n

**13.** **A.** Kibe anapenda kucheza mchezo wa kibe **B.** akutanguliaye chanoni hukuzidi tonge
**C.** amenenepa kama hanziri **D.** kilimo ni uti wa mgongo

**14.** **A.** huruma **B.** huzuni **C.** fahari **D.** shufaka

**15.** **A.** $\frac{7}{8}$ **B.** $\frac{8}{7}$ **C.** $\frac{3}{8}$ **D.** $\frac{5}{8}$

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** **Andika wingi wa sentensi ifuatayo**

*Ukuta ule aliokujengea una ufa.*

A. Kuta ile alizokujengea ina nyufa.

B. Nyuta zile mlizowajengea zina nyufa.

C. Kuta zile walizomjengea zina nyufa.

D. Kuta zile walizomjengea zina nyufa.

**17.** **Upi ni ukanusho sahihi wa**

*Zuhura alikuwa akiwapokea na kuwakaribisha wageni*

A. Zuhura hakuwa akiwapokea na kuwakaribisha wageni.

B. Zuhura hakua akiwapokea wala kuwakaribisha wageni.

C. Zuhura alikuwa hawapokei ila kuwakaribisha wageni.

D. Zuhura alikuwa hapokei bali kuwakaribisha wageni.

**18.** **Chagua usemi wa taarifa wa**

*Komu alimwabia bintiye, "Tukimaliza kazi utaenda mjini*

A. Komu alimwambia bintiye kuwa wangeenda mjini wakimaliza kazi.

B. Komu alimwambia bintiye kuwa wangemaliza kazi angeenda mjini.

C. Komu alimwambia bintiye angemaliza kazi wangeenda mjini.

D. Komu alimwambia bintiye amalize kazi waende mjiji.

**19.** Ipi ni tofauti ya maana kati ya watatu na wa tatu?

A. Watatu ni idadi ya jumla lakini wa tatu ni idadi katika orodha.

B. Watatu ni idadi kamili lakini wa tatu ni idadi ya jumla.

C. Watatu ni idadi ya makadirio lakini wa tatu ni idadi kamili.

D. Watatu ni idadi kamili lakini wa tatu ni anayechukua nafasi ya tatu katika orodha.

**20.** Kanga ni vazi la kike. Kanga pia ni

A. mnyamapori jamii ya mamba.

B. kuivisha kitu kwenye mafuta.

C. ndege wa porini jamii ya kuku.

D. ndege wa ziwani mwenye madoa.

**21.** **Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa**

*Salome alienda uwanjani akacheza mpira*

A. Mpira ulichezwa na Salome uwanjani.

B. Salome aliuchezea mpira uwanjani.

C. Mpira ulichezewa uwanjani na Salome.

D. Uwanjani ulichezwa mpira na Salome.

**22.** Upi ndio muungano mwafaka wa

*(i) Sitojali anaugua macho*

*(ii) Sitojali alisoma barua*

A. Sitojali anaugua macho bali pia alisoma barua.

B. Sitojali anaugua macho ilhali alisoma barua.

C. Sitojali ingawa anaugua macho alisoma barua.

D. Sitojali alisoma barua ijapo anaugua macho.

**23.** Chagua maelezo sahihi

A. Arbuni ni sehemu ya malipo ya kukopea mwanzoni.

B. Riba ni pesa za ziada kwa mkopo.

C. Kiinuamgongo ni malipo anayopewa mtu ili ajiuzulu.

D. Masrufu ni pesa za kufanya kazi ya ziada.

**24.** Akisami $\frac{5}{9}$ huandikwaje kwa maneno

A. Humusi tisa.

B. Humusi tano.

C. Tusui tano.

D. Tusui tisa.

**25.** Orodha ipi ina vitenzi pekee?

A. Dhaifu, laini, tele, geni.

B. Polepole, sanasana, haraka, kwa kiasi.

C. Ijapokuwa, mighairi ya, ilhali, na

D. Lima, jenga, chupa, oga.

**26.** Halaiki ya watu, thurea ya nyota na kikoa cha waimbaji ni mfano wa nomino

A. za jamii.

B. dhahania.

C. ambata.

D. jumuishi.

**27.** **Tambua maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo**

*Darasa <u>hilo</u> limejengwa <u>**karibu na**</u> barabara.*

A. Kivumishi, kihusishi.

B. Kivumishi, kiwakilishi.

C. Kivumishi, kiunganishi.

D. Kiwakilishi, kivumishi.

**28.** Jina 'halikadhalika' lina silabi ngapi?

A. 6

B. 13

C. 12

D. 8

**29.** Mtoto wa nzige huitwaje

A. Kiyoyo.

B. Kinengwe.

C. Kingonyo.

D. Kimatu.

**30.** Ni sentensi gani iliyotumia kwa kuonyesha sababu?

A. Wanafunzi walifaulu kwa bidii zao.

B. Kusoma kwa bidii kuliwasaidia wanafunzi.

C. Kusoma kwa wanafunzi kuliwasaidia kufaulu.

D. Wanafunzi walisomea kwa wazazi wao.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Kila mgombea urais, anataja vile ambavyo atapambana na jinamizi la ufisadi. ***Japo kwangu naona zao ni ahadi za Kiswahili,*** jinamizi hili linafaa kukabilianwa nalo bila huruma. Shida ya vita hivi vya ufisadi kwa sasa ni kuwa, vimetawaliwa na siasa. Raia wa mrengo fulani wanaamini kuwa ni fulani tu aliye na uwezo wa kuangamiza ufisadi. Hili ni tatizo kubwa kwa kuwa athari za ufisadi huwa hazichagui kabila, rangi, dini au mirengo ya siasa. Hivyo basi, ombi langu ni kuwe na kiongozi mwenye haki ambaye hatashurutishwa au kuingiliwa kisiasa.

Ukweli ni kuwa, ufisadi umekuwako tangu jadi. Kiini hasa cha ufisadi ni tamaa. Hili ni jambo ambalo ni kinyume na maadili au kawaida za jamii. Hebu sasa tuangamize madhara ya ufisadi.

Ufisadi umechangia sana kuwa na maendeleo duni. Kutolewa kwa kiasi fulani cha fulusi kama hongo ni kiini mojawapo cha kuwepo na maendeleo uchwarauchwara. Hii ni kutokana na ukweli kuwa rushwa husababisha kupunguzwa kwa kiasi cha fedha za kutekeleza miradi mbalimbali. Si ajabu wafanyakazi wa kutekeleza miradi mbalimbali kukosa kulipwa au kupunjwa kwa kupewa mshahara wa kijungujiko, kukosa kulipwa au hata kulipwa nusu ya mshahara. Hili ni jambo linalovunja moyo; hivyo kutojitahidi kazini.

Hebu angalia maeneo mbalimbali nchini. Kila mahali visa vya ***ubadhirifu*** wa pesa zilizotengewa miradi mbalimbali zimeripotiwa. Mara nyingi jambo hili hutendwa na wasimamizi wa hazina ya maendeleo. Kwa mfano ni jambo la kuvunja moyo kuona baadhi ya watumishi wa umma wakitumia pesa za maendeleo katika safari za kuzuru mataifa ya nje. Safari hizi huwa hazina manufaa yoyote kwa raia ila kwa wahusika. Viongozi kama hawa huongozwa na ubinafsi na tamaa iliyokithiri mipaka. Viongozi kama hawa wanafaa kukumbushwa kuwa tamaa ilimwua fisi. Matokeo yake ni ukosefu wa huduma muhimu kwa wananchi.

Ufisadi umechangia kwa kiwango kikubwa uchipuzi wa miradi ya kiwango cha chini. Hali hii huchangiwa kutokana na utumizi wa malighafi ghushi. Ukweli ni kuwa miradi inayotekelezwa hudumu katika hali nzuri kwa mwia mfupi tu. Baada ya muda mfupi, ukarabati huanza. ***Ajabu ni kwamba, ukarabati huu huishia kutumia pesa nyingi kuliko mradi wenyewe***. Je, huu n ungwana?

Tumeona mataifa tajiri hususan yale ya magharibi yakidinda kufadhili miradi hapa nchini. Ukiwauliza wanasema kuwa, hakuna uwazi katika matumizi ya pesa za umma. Matokeo ya haya ni miradi muhimu hukosa kufanyika na hali hii huzidisha uchochole miongoni mwa raia. Japo uamuzi wa mataifa haya ni mzuri, ukweli ni kuwa wananchi ndio huteseka.

Nikimalizia, shida nyingine ni ile ya kuwapiga konde la nyuma waliotwikwa dhima ya kukagua iwapo miradi imefikia kiwango kinachostahili. Ulaji rushwa huchangia maendeleo duni. Uidhinishaji huu huishia kuleta athari hasi kama vile kuporomoka kwa majengo na kuhiliki maisha ya ~~watu wasio~~ na makosa, kutumia pesa nyingi katika ukarabati na kufanya raia wengi kukosa ajira na hivyo wanashindwa kujimudu kimaisha. Rushwa pia imesababisha ulemavu kwa kuwa jumba ikiporomoka viungo vya mwili huweza kuvunjika.

Vita dhidi ya ufisadi, havifai kuachiwa dola pekee. Kila mmoja ana jukumu lake na mchango wake. Dhana kuwa hakuna linalowezekana bila rushwa inafaa kuzikwa katika kaburi la liliwala.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, shida kubwa inayoathiri vita dhidi ya ufisadi ni

A. kila mkenya anashiriki ufisadi kwa njia moja au nyingine.
B. kila mtu anayetaka kuchaguliwa kuwa rais anaelezea vile ambavyo atapambana na ufisadi.
C. siasa zimeingizwa katika vita hivi na kufaulu hutegemea mirengo ya kisiasa.
D. hakuna mtu yeyote ambaye hajafisidi katika shughuli zake za kimaisha.

**32.** Ni nini maana ya kauli hii?
Japo kwangu naona zao ni ahadi za Kiswahili

A. Msimulizi anaona ahadi hizo zikiwa za uongo.
B. Msimulizi anaamini kuwa ahadi hizo zitatekelezwa.
C. Msimulizi anaonelea ahadi hizo zitolewe kwa lugha ya Kiswahili ili Wakenya wengi waelewe.
D. Msimulizi anaonelea ahali hizo zingetolewa kwa wote wanaoelewa lugha ya Kiswahili.

**33.** Ufisadi husababisha yote yafuatayo ila

A. wafanyikazi kulipwa mishahara nusu.
B. wafanyakazi kulipwa mishahara ambayo haiwezi kuwasaidia kujikimu.
C. wafanyikazi kufanya kazi na kukosa mishahara.
D. Kujitolea kazini na kuwa na matokeo bora.

**34.** Viongozi wanaofanya safari za mataifa ya nje

A. huwa wanaongozwa na tamaa na ubinafsi.
B. huwa wanaongozwa na mapenzi ya kutaka kuwasaidia wananchi.
C. huwa hawajazuru mataifa mengi wakilinganishwa na wenzao kutoka katika mataifa mengine.
D. lengo lao huwa ni kujifunza udhaifu na matatizo yanayojichipuza katika kazi zao.

**35.** Jina ubadhilifu lina maana ya

A. wizi wa pesa za umma.
B. utumizi mbaya wa pesa za umma.
C. ulipaji wa pesa za umma.
D. utumizi wa pesa za umma.

**36.** Ikiwa miradi duni itaidhinishwa kutekelezwa

A. gharama kubwa itatokea wakati wa ukarabati.
B. miradi iliyoanzishwa haitaonekana kamwe.
C. viongozi walioidhinishwa watajipata wakitumikia vifungo vya maisha gerezani.
D. pesa nyingi zitatumika kukamilisha miradi husika.

**37.** Hii ni tamathali gani ya lugha?
*Ajabu ni kwamba ukarabati huu huishia kutumia pesa nyingi kuliko mradi wenyewe.*

A. Chuku.
B. Kinaya.
C. Istiari.
D. Tashhisi.

**38.** Madhara makuu zaidi yanayosababishwa na ufisadi kwa mujibu wa kifungu hiki ni

A. kufaidika kwa wachache huku wengine wakiendelea kuumia.
B. wananchi kukosa huduma muhimu kama za matibabu.
C. utumizi mbaya wa rasilimali za umma.
D. vifo vya watu wasiokuwa na hatia.

**39.** Mataifa ya magharibi kabla ya kufadhili miradi nchini

A. lazima yapewe hongo kwanza.
B. lazima yajue ni miradi gani inayotekelezwa.
C. lazima pawe na uwajibikaji wa hali ya juu.
D. lazima pawe na uhusiano mwema na mataifa husika.

**40.** Katika aya ya mwisho, msimulizi anatoa wito kuwa

A. ufisadi utaendelea kuliangamiza taifa.
B. viongozi wa kisiasa waache kabisa kutumia hongo katika shughuli za umma.
C. mchango wa kila mmoja ni muhimu ili kukabili ufisadi.
D. maneno matupu hayatoshi kukabiliana na ufisadi.

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Tapeli alikuwa danga la mwana. Zaidi ya hayo, aliweza kujaliwa kichwa chepesi. Hali hii ilimsaidia kutatua mambo ambayo hata walimu wengine waliyaona mlima. Kutokana na ukweli huu, hata wenzake waliweza kumvulia kofia kwa busara hii. Walimu walikuwa wakishindwa kwa nini migogoro mingi haikuweza kuwafikia kumbe ilikuwa ikitatuliwa na Tapeli. Kwa haya, Tapeli akawa amejishindia nafasi kubwa nafsini mwa wenzake.

Waswahili husema hakuna mchele ukosao ndume. ***Kumbe Tapeli alikuwa amewafichia wenzake kucha.*** Hakuwa tayari kupokea lawama za aina yoyote ile. Angekosea hata kosa la kibinadamu, aliwalimbikizia wenzake. Hii ilimaanisha kuwa mizigo yake mingi aliwabebesha wenzake. Hapo wengi wakamwona kama kitatange wa kuwachunjia wenzake demani . Sijui kwa nini akaona ugumu wa kukosea ilhali wahenga husema kosa ni kurudia kosa si kukosa.

Kwa kuwa Tapeli alikuwa kijana mwenye bidii za mchwa, aliweza kukamilisha masomo yake na kufaulu. Kibarua kikawa ni kusaka ajira. Hakuwa na bahati kwa kuwa viatu vyake vilibusu lami mpaka soli ikamalizika. Alikuwa akibisha mlango mmoja hadi mwingine bila bahati kumwangukia.

Tapeli kuona jinsi ya kupata kazi ilikuwa kibarua, [illegible] kichwa. Alisema mwana akikosa titi la mama hata la mbwa huamwa. Katika akiba yake, alikua na hela kidogo. [illegible] kukodisha chumba kimoja mjini na kukipamba kwa samani aali aali. Chumba hicho kikawa ofisi yake. Naye akajitwika wadhifa wa kuwa mkurugenzi mkuu. Aliwatafuta vijana wanne na kuwaajiri katika 'shirika' lake. Ofisi ile ilifanyika ***wakala*** wa kutafutia vijana kazi katika mataifa ya Mashariki na Mashariki ya kati. Ili kuweza kuwafikia watu wengi, alichapisha matangazo kwenye magazeti na kupeana nambari zake za simu. Vilevile alitumia mitandao ya kijamii ya Twita. Vijana nao walifurika kama kumbikumbi kuisaka ajira hii.

Ajira hii haikuwa waipate bila malipo. La hasha! Kila kijana alitakiwa kulipa ada ya shilingi elfu hamsini. Pesa hizi ziligharamia mahitaji yote yaliyotakikana. Ili kuweza kuwavutia vijana wengi, Tapeli aliweza kuweka pasipoti mitandaoni. Kitendo hiki tu kilifanya wengi hata kukopa ili waweze kwenda Uarabuni.

Naam, Tapeli alichukua kijana mmoja tu na kumpeleka hadi katika uwanja wa ndege ili aelekee Uarabuni. Alipiga picha nyingi sana na kuziweka mitandaoni. Kile wengi hawakujua, kijana huyu alikuwa mshirika wake wa karibu. Lakini lengo lao lilitimia pale mamia ya vijana walipoomba nafasi za kuelekea Uarabuni. Pesa nazo zikanyesha kama mvua. Tapeli akalala hohehahe na kuamka akinuka pesa.

Jamaa wengi walifilisika. Kuna hata wale waliuza mifugo ili kupata pesa za usajili. Mikopo nayo ikaongezeka. Mali nyingi ikawekwa rehani yakiwemo mashamba ya watu. Ajabu huajabiwa. Siku moja kuna wale waliofika 'ofisini' wakakuta imefungwa. Wakarejea siku iliyofuata lakini siku iliyofuata, waliona bango kubwa limepigiliwa juu ya mlango /**CHUMBA CHA KUPANGA. NAMBARI YA:8086945672434**/. Hapo ndipo ilipobainika kuwa, Tapeli alikuwa amewatapeli. ***Hata hivyo mkono mrefu wa serikali uliweza kumpata na kwa sasa anakula kalenda katika gereza kuu la REKEBISHA TABIA.***

**41.** Chagua kauli isiyo ya kweli kulingana na aya ya kwanza

A. Tapeli alikuwa mtoto aliyelelewa vizuri na wazazi wake.
B. Tapeli alikuwa akiheshimiwa sana na wenzake.
C. Tapeli alikuwa akikaa katika nafsi za wenzake wavulana.
D. Ni migogoro michache sana iliweza kuwafikia walimu.

**42.** Ni nini maana ya kauli ifuatayo:
*Kumbe Tapeli alikuwa amewafichia wenzake kucha*

A. Tapeli alikuwa akikata kucha zake wakati alikuwa amejificha.
B. Tapeli alikuwa ameficha tabia zake halisi.
C. Tapeli hakuwa na lawama zozote kwa wengine.
D. Tapeli kwenye vidole hakuwa na kucha kumbe alikuwa amezikata.

**43.** Kulingana na kifungu, kwa nini ilikuwa vigumu kupata ajira?

A. Ni wazi kuwa Tapeli hakuwa amehitimu vizuri.
B. Nafasi za ajira zilikuwa adimu.
C. Hakuwa na uwezo wa kuzuru ofisi nyingi.
D. Tapeli alikuwa akipenda sana kubagua kazi.

**44.** Tapeli alimaanisha nini aliposema kuwa, *"Mwana akikosa titi la mama hata la mbwa huamwa"*

A. Kwa kawaida mtoto anayekosa maziwa ya kawaida anaweza kunyonyeshwa mbwa.
B. Kwa kawaida kazi bora ni vigumu sana kupatikana iwapo huna elimu.
C. Kazi nyingi za maana huwa ni za wale wamesoma.
D. Alipokosa kazi ya hadhi, alikuwa tayari kufanya yoyote iliyopatikana.

**45.** Maana ya ***wakala*** ni

A. Ajenti.
B. Ajenda.
C. Dhima.
D. Kaimu.

**46.** Matumizi ya Twita

A. yalimfanya Tapeli kutoweza kufikia watu wengi jinsi alivyotaka.
B. yalimsaidia Tapeli kuweza kufikia watu wengi.
C. ndiyo yaliyosambaratisha juhudi zake za kuwalaghai watu.
D. yalimsaidia Tapeli kupata kazi aliyokuwa amesomea chuoni.

**47.** Unadhani ni kwa nini Tapeli aliweza kumsindikiza mhusika mmoja hadi kwenye uwanja wa ndege na kupiga picha alizotuma mitandaoni?

A. Alikuwa ameamua kuwapeleka wote waliotuma maombi katika mataifa ya Mashariki ya kati.
B. Alidhamiria kutumia picha hizo kama chambo cha kuwanasia wateja zaidi.
C. Vijana wengi walimshuku na picha hizi zingeweza kuwathibitishia wote.
D. Ndoto yake ya kufika katika mataifa ya Mashariki ya kati ilikuwa imetimia.

**48.** Kwa nini wote waliofika 'ofisini' hawakuweza kumpata Tapeli?

A. Nafasi za ajira zilikuwa zimeisha katika Mashariki ya kati.
B. Alikuwa ametoweka baada ya kuafikia malengo yake ya kuwapuja watu hela zao.
C. Tapeli alikuwa amesafiri kuenda ughaibuni kukagua hali ya maisha.
D. Alikuwa ametoweka kwenda kufungua akaunti ya kuweka pesa alizokusanya kutoka kwa watu.

**49.** Ni methali gani inayoweza kujumuisha ujumbe uliopigiwa kistari
***Hata hvyo mkono mrefu wa serikali uliweza kumpata na kwa sasa anakula kalenda katika gereza kuu la REKEBISHA TABIA.***

A. Mbio za sakafuni huishia ukingoni.
B. Akili ni nywele kila mtu ana zake.
C. Yote yang'aayo si dhahabu.
D. Mkono usioweza kuukata ubusu.

**50.** Tapeli akalala hohehahe akaamka akinuka pesa. Hii

A. inaonyesha mateso ambayo Tapeli alipitia maishani.
B. inaonyesha kuwa. Tapeli alipenda sana kulala.
C. inaonyesha n[illegible] mfupi ambao Tapeli alitumia kuta[illegible]
D. inaonyesha k[illegible]peli alikuwa akihitaji pesa.